

Matibabu ya Ugonjwa wa Malaria

Malaria ni ugonjwa unaoathiri watu wengi sana nchini Tanzania. Watu wengi wanaoenda katika vituo vya kutolea huduma ya afya wanaogua ugonjwa wa malaria.

Ugonjwa wa malaria umezoeleka sana kiasi kwamba watu wanadhani kwamba hauwezi kuepukika. Hii siyo kweli. Ugonjwa wa malaria unazuilika na kutibika.

Dalili za ugonjwa wa malaria

- Mwili kuwa na joto kali
- Kuhisi baridi na kutetemeka
- Maumivu ya kichwa, mwili au viungo
- Kichefuchefu au kutapika
- Kukosa hamu ya kula
- Maumivu ya tumbo, kuharisha
- Mtoto kushindwa kunyoya

Ni muhimu kuzifahamu dalili za malaria. Iwapo utaona mojawapo au zaidi ya dalili hizi za malaria unatakiwa kuwahi kwenye kituo cha kutolea huduma ya afya ndani ya saa 24 tangu uanze kuona dalili hizo.

Mtoa huduma za afya atakufanyia vipimo kuangalia kama una vimelea vya malaria au una ugonjwa mwingine. Iwapo utgundulika kuwa na vimelea vya ugonjwa wa malaria, mtoa huduma za afya atakupata dawa mseto ya malaria

Umuhimu wakupata matibabu ya malaria mapema

Manufaa za kupata matibabu ya ugonjwa wa malaria mapema ni kama yafuatayo:

- Kupunguza hatari ya kupata malaria kali inayoweza kusababisha ulemavu au kifo
- Kukatiza mzunguko wa maambukizi ya malaria. Ukitibiwa malaria haraka, ndivyo unavyokatiza haraka mzunguko wa maambukizi. Mbu akimuuma mtu asiye na maambukizi ya malaria hataweza tena kuchukua vimelea vya malaria na kuambukiza mtu mwingine
- Kuepuka gharama za juu za matibabu ya malaria kali
- Kupunguza uwezekano wakupoteza kipato au mtoto kukosa masomo mara kwa mara

Tiba sahihi ya ugonjwa wa malaria

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imependekeza Dawa mseto ya malaria kutibu malaria. Dawa mseto ni mchanganyiko wa dawa mbili au zaidi ambazo huifanya kuwa na nguvu ya kutibu kwa kiwango cha juu, kwa haraka na ni salama.

- Dawa mseto inapatikana kwenye vituo vyote vya afya na kwenye duka lolote la dawa lililo karibu na wewe.
- Dawa mseto zinapatikana kwenye vituo vya afya na maduka ya dawa kwa bei nafuu. Dawa hizi zimefunguzwa bei na serikali ili kumuwezesha mtu wa kawaida kuzinunua kwa ajili ya matibabu ya malaria.
- Kwa sasa, utazitambua dawa mseto kwa kuangalia alama ya jani lililopo kwenye pakiti ya Dawa Mseto.
- Watu wenye mahitaji maalum kama wasioona au viziwi, ni vyema wakapewa maelekezo ya kina kuhusu kuitambua dawa mseto

Umuhimu wa kumaliza dozi ya Malaria

Ni muhimu sana kumeza dawa zote kama ulivyoelekezwa na mtoa huduma za afya ili upone malaria na isikurudie mara kwa mara.

Unaweza kuanza kujisikia nafuu baada ya kumeza vidonge vichache na ukaacha kumaliza dozi. USIFANYE HIVI, ni hatari sana. Inawezekana bado ukawa na vimelea vya malaria katika damu yako.

Athari za kutomaliza dozi ya malaria:

- Utarudia kuumwa tena
- Itasababisha vimelea vya malaria kuwa sugu kwa dawa na kutopona haraka

Vitu muhimu vya kueleza jamii kuhusu matibabu ya malaria

Yafuatayo ni mambo ya muhimu ya kueleza jamii kuhusu matibabu ya ugonjwa wa malaria

- Malaria inatibika, wahi kituo cha kutolea huduma ya afya mara tu unapohisi dalili za malaria ili upate matibabu
- Ni muhimu kupata matibabu ya ugonjwa wa malaria mapema
- Dawa mseto ndiyo tiba sahihi ya ugonjwa wa malaria
- Dawa mseto zinapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma ya afya na kwenye maduka yote ya dawa kwa bei nafuu, unayoweza kuimudu
- Utaitambua Dawa Mseto kwa kuangalia alama ya jani la kijani kwenye pakiti ya dawa
- Hakikisha unameza dawa zote kama ulivyoelekezwa na mtoa huduma za afya ili upone malaria



Matibabu ya Ugonjwa wa Malaria

